# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Tatu




Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Tatu



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1117

Jina la Chapisho: Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-877-4

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 23 Oktoba, 2023 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Tatu katika Ngazi ya Elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2023.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI DARASA 3.indd 1 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2018
Chapa ya Pili 2021
Toleo la Pili 2023

ISBN: 978-9987-09-877-4

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 168 / +255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 2 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Shukurani** .................................................. v

**Utangulizi** .................................................. vi

**Sura ya Kwanza**
Sauti za herufi mwambatano .................................................. 1

**Sura ya Pili**
Kuzungumza .................................................. 11

**Sura ya Tatu**
Kutumia msamiati .................................................. 16

**Sura ya Nne**
Visawe na vinyume .................................................. 21

**Sura ya Tano**
Methali, nahau na vitendawili .................................................. 31

**Sura ya Sita**
Alama za uandishi .................................................. 42

**Sura ya Saba**
Kusikiliza mazungumzo .................................................. 52

**Sura ya Nane**
Kutumia kamusi .................................................. 57

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 3 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Tisa**
Kusoma kwa ufahamu na ufasaha ....................................... 64

**Sura ya Kumi**
Ninaweza kuandika ........................................................... 70

**Sura ya Kumi na Moja**
Kuchambua matini ............................................................ 75

**Sura ya Kumi na Mbili**
Kusimulia hadithi ............................................................. 79

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 4 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki kutoka taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali zilizoshiriki kufanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi. Kipekee TET inatoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, Vyuo vya Ualimu na Shule za Msingi. Pia, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

**Waandishi:** Bi. Rose S. Chipindula, Dkt. Tulia Michael na Bi. Sarah Msafiri

**Wahariri:** Dkt. Saul S. Bichwa, Dkt. Adventina Y. Buberwa na Bw. Aaron J. Mweteni

**Msanifu:** Bw. Silvanus A. Mihambo

**Wachoraji:** Bw. Fikiri A. Msimbe, Bw. Yohana P. Mwenda na Bw. Gwakisa U. Mwandoloma

**Mratibu:** Bi. Rose S. Chipindula

Vilevile, TET inatoa shukurani kwa walimu wote wa shule za msingi na wanafunzi walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Mwisho, TET inaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zilizofanikisha kazi ya uandishi na uchapishaji wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
***Taasisi ya Elimu Tanzania***

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 5 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu cha Kiswahili Darasa la Tatu kimetayarishwa kwa kuzingatia Muhtasari wa Somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la Tatu mpaka la Sita wa Mwaka 2023 uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, Kitabu hiki ni Toleo la Pili lililoboreshwa kutoka kitabu cha Kiswahili kilichochapishwa Mwaka 2018 kwa kuzingatia mtaala wa Mwaka 2016.

Lengo la kitabu hiki ni kukuza uwezo wako wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika Kiswahili. Pia, kitakuwezesha kutumia msamiati wa lugha ya Kiswahili kwa namna mbalimbali. Vilevile, kitakujengea uwezo wa kupanga mawazo yako kwa mpangilio na mtiririko unaotakiwa.

Kitabu hiki kina hadithi, habari, mashairi, ngonjera, maigizo na majigambo. Vyote hivi vitakuwezesha kujifunza kwa ufasaha. Pia, kina maswali ya kupima ufahamu wako kutokana na ulichokisikiliza, ulichokiona au ulichokisoma. Vilevile, kina mazoezi mbalimbali yatakayokuwezesha kujenga ujuzi wako wa somo la Kiswahili.

Soma kwa makini kitabu hiki ili uweze kujenga ujuzi wako wa kumudu somo la Kiswahili.

Jifunze zaidi kupitia maktaba mtandao
*https://ol.tie.go.tz* au *ol.tie.go.tz*

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 6 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Sauti za herufi mwambatano

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Pili ulijifunza kutamka sauti mbalimbali za herufi mwambatano. Katika sura hii, utajifunza namna ya kutamka sauti za herufi mwambatano* ***ngw****,* ***ndw****,* ***njw****,* ***mbw*** *na* ***nzw*** *katika silabi, maneno, sentensi na habari. Umahiri utakaoujenga baada ya kujifunza sauti hizi utakusaidia kuwasiliana katika miktadha mbalimbali.*

**Fikiri**

**Aina za herufi katika shairi hili**

Siku yetu ya thamani, darasa jipya lang'aa,
Madawati yasheheni, uhakika wa kukaa,
Wote twasoma rahani, walimu nao wafaa,
Furaha iso kifani, la tatu tumeingia.

**Ufahamu**

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Darasa jipya**

Ndwamila na Ndwalima ni marafiki. Wote wanasoma katika Shule ya Msingi Pongwe. Mwaka jana walikuwa Darasa la Pili.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwaka huu wameingia Darasa la Tatu. Shule ya Msingi Pongwe ilifunguliwa wiki ya kwanza ya mwezi Januari. Siku ya kufungua shule ilikuwa kama siku ya kufungwa kwa shule. Wanafunzi wengi walifika shuleni mapema isipokuwa wachache waliokuwa na changamoto ikiwemo ugonjwa. Wanafunzi waliofika shuleni walifanya usafi wa mazingira. Mazingira ya shule yanapaswa kutunzwa na kila mwanafunzi. Baadaye, kengele iligongwa na wanafunzi wakaenda mstarini.

Mwalimu Mbwete alikuwa mwalimu wa zamu. Aliwasalimia wanafunzi na kuwatakia **heri** ya mwaka mpya. Aliwaeleza kuwa kila mwanafunzi anapaswa kusoma kwa **bidii**. Aidha, anapaswa kuzingatia sheria za shule. Aliwaeleza wanafunzi kuwa vyumba vya madarasa vimebadilika. Kila mwanafunzi atapangwa katika darasa lake. Wanafunzi waliokuwa Darasa la Kwanza mwaka uliopita, wataingia **chumba** cha Darasa la Pili. Wanafunzi waliokuwa Darasa la Pili wataingia chumba cha Darasa la Tatu. Baada ya matangazo, wanafunzi waliingia madarasani kwa **mbwembwe**.

Wanafunzi wa Darasa la Tatu walianza mwaka wakiwa na furaha. Kila mwanafunzi alikuwa na hamu ya kuanza kusoma katika darasa jipya. Walipoingia darasani, mwalimu wa darasa aliwaongoza kuchagua **viranja** wa darasa. Wanafunzi wanne walijitokeza kugombea nafasi hizo, wawili walishinda na wengine wawili walishindwa katika uchaguzi huo. Ndwamila alichaguliwa kuwa dada wa darasa na Ngwile kaka wa darasa.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 2 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Ndwamila na Ndwalima wanasoma shule gani?
2. Shule ilifunguliwa lini?
3. Taja sababu ya baadhi ya wanafunzi wachache kutokufika shule.
4. Kwa nini wanafunzi wa Darasa la Tatu walikuwa na furaha?
5. Taja herufi mwambatano zilizotumika katika habari hii.
6. Bainisha maneno yenye sauti za herufi mwambatano **ngw**, **ndw**, **njw**, **mbw** na **nzw** katika habari hii.
7. Umejifunza nini kutokana na habari hii?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 3 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana za maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano:** **chumba** - *sehemu iliyogawanywa ndani ya jengo*
*Chumba cha darasa letu kimedekiwa.*
*Kila siku ninasafisha chumba changu.*

1. heri
2. bidii
3. chumba
4. mbwembwe
5. kiranja

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Soma maneno yafuatayo kwa sauti na haraka:**

pangwa, chungwa, fungwa, tingwa, pingwa, shindwa, tendwa, undwa, pendwa, lindwa, chanjwa, chinjwa, vunjwa, kunjwa, funzwa, tunzwa, ombwa

**B. Soma sentensi zifuatazo kwa sauti na haraka:**

(i) Wafungwa hulindwa popote wanapokuwa.
(ii) Timu ya Kimbwe ilifungwa magoli mawili kwa moja.
(iii) Turubai lilikunjwa na kufungwa kwa kamba.
(iv) Mtumbwi wa babu umegongwa na ngalawa.
(v) Mgonjwa alishindwa kula machungwa.
(vi) Watoto hulindwa wakati wote.
(vii) Kinga ilinikinga na magonjwa ya kuambukizwa.
(viii) Nyumba iliyojengwa na Musa ilivunjwa kwa urahisi.
(ix) Ufunguo uliochongwa na Doto hauvunjwi na kitu chochote.
(x) Tausi ni ndege anayetembea kwa mbwembwe.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 4 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**C. Unda maneno kumi kwa kutumia jedwali lifuatalo:**

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | T | U | M | B | W | I | T |
| B | G | A | F | CH | E | CH | E |
| W | U | O | U | I | T | U | I |
| E | N | M | N | N | U | N | G |
| M | D | B | G | J | M | G | A |
| B | W | W | W | W | E | W | E |
| W | A | A | A | A | K | A | A |
| E | M | F | U | N | Z | W | A |

**Mfano:** MTUMBWI

**D. Oanisha picha zilizopo sehemu A na majina yake katika sehemu B.**

| Na. | Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|---|
| (i) |  | dimbwi |
| (ii) |  | fyekeo |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | | |
|---|---|---|
| (iii) |  | chungwa |
| (iv) |  | mwanafunzi |
| (v) |  | mtumbwi |

**E. Chagua herufi ya jibu sahihi.**

(i) Tunasafisha _______ kila baada ya mlo.

(a) mwili

(b) kinywa

(c) meno

(d) fizi

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 6 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Mtoto mtiifu ________ vizuri na jamii yake.
   (a) anafunza
   (b) amefuzu
   (c) amefunzwa
   (d) amefaulu

(iii) Jongoo ________ na miguu mingi.
   (a) amefinyangwa
   (b) ametengenezwa
   (c) ameumbwa
   (d) amejengwa

(iv) Chungu cha bibi ________ kwa udongo mwekundu.
   (a) kimefinywa
   (b) kimefinyangwa
   (c) kimefinyanga
   (d) kimeumbwa

(v) Kitanda chetu ________ kwa chuma.
   (a) kimetengeneza
   (b) kimetengenezeka
   (c) kimetengenezesha
   (d) kimetengenezwa

(vi) Koti la babu limeliwa na ________.
   (a) kunguni
   (b) mchwa
   (c) chawa
   (d) kiroboto

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 7 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vii) Tochi ya kaka ina _______ mzuri.

(a) mwanga
(b) umbo
(c) miale
(d) nuru

**F. Andika umoja na wingi wa maneno yafuatayo:**

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| **Mfano:** | mtoto | watoto |
| (i) | mbweha | __________ |
| (ii) | __________ | madimbwi |
| (iii) | mtumbwi | __________ |
| (iv) | __________ | waungwana |
| (v) | ngwara | __________ |
| (vi) | ngedere | __________ |
| (vii) | __________ | miamba |
| (viii) | bingwa | __________ |

**G. Tunga sentensi kumi kwa kutumia jedwali lifuatalo, kisha soma sentensi hizo kwa sauti.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mpira<br>Wanafunzi<br>Mzee Mbwete<br>Mlimbwende<br>Mboga<br>Kengele<br>Darasa<br>Mbuzi | alimdondosha<br>ulichezwa<br>alichinjwa<br>iliungwa<br>hufunzwa<br>limepambwa<br>iligongwa<br>hupendwa<br>aliingia | kwa<br>na | ngwara<br>karanga<br>watoto wote<br>kisu<br>picha<br>mbwembwe<br>walimu |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**H. Panga sentensi zifuatazo kwa mtiririko:**

(i) Ngozi yake imeundwa kwa rangi nyingi nzuri ambazo hubadilikabadilika.

(ii) Hakika kinyonga ni mnyama aliyefunzwa kutembea kwa mbwembwe.

(iii) Anapowaona watu, hutembea kwa haraka kwani anaogopa kujeruhiwa.

(iv) Rangi hizo humsaidia kujilinda na maadui ili asionekane.

(v) Kinyonga ni mnyama muungwana na mwema sana.

## Kazi ya kufanya

**Soma igizo lifuatalo, kisha igiza.**

**Kiongozi** Karibuni wote tunawaletea igizo la mashabiki wa mpira. *(Kiongozi anaondoka, Amani, Upendo na Mwamvua wanaingia.)*

**Amani** Upendo, si nilikwambia kuwa sisi tutakuwa washindi kwenye mashindano ya mpira wa miguu? Hahahaaa...!

**Upendo** Loo! Ushindi wenyewe mliubahatisha. Ndiyo tulishindwa lakini si tulipewa zawadi za kushiriki?

**Mwamvua** Heheheee...! Usinichekeshe Upendo, mimi nilijua tu mtafungwa kuanzia magoli mawili na kuendelea.

**Upendo** Uwiiii...! Ulijuaje?

**Mwamvua** Wewe! Si niliwaona wachezaji wenu wanavyokimbia uwanjani kama wagonjwa.

**Amani** Ndiyo! Mwamvua ni kweli hata mimi niliona hivyohivyo.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 9 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Upendo** Ndugu zangu, tuliponzwa na mlinda lango wetu. Alikuwa na mbwembwe nyingi sana. *(Wote wanatawanyika huku Amani na Mwamvua wakiwa na furaha na Upendo akiwa na huzuni.)*

## Zoezi la 4: Utungaji

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwenye aya ifuatayo kwa kutumia maneno uliyopewa:**

kutunzwa, mbwembwe, mtumbwi, alichinjwa, alishindwa, machungwa, mbwa, walikaangwa

Siku moja baba alielekea ziwani akapanda ________ kwenda kuvua dagaa. Baada ya kutoka ziwani alinunua ________ akayapeleka nyumbani. Wote tulimpokea kwa ________ huku tukifurahia zawadi alizotuletea. Dagaa ________ vizuri na ________ kwenye kikapu. Kaka ________ kumpa mbwa dagaa kwa kuwa mbwa wetu hapendi kula dagaa. Bahati nzuri ng'ombe wa jirani ________. Hivyo, kaka alikwenda kwa jirani kuchukua mifupa kwa ajili ya ________wetu.

FOR ONLINE USE ONLY

# Sura ya Pili

## Kuzungumza

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kuzungumza kwa kuzingatia kupanda na kushuka kwa sauti. Utaweza kubadili sauti kulingana na hisia au muktadha wa mazungumzo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuanzisha na kuendeleza mazungumzo kwa kujiamini katika miktadha mbalimbali.*

### Fikiri

Namna unavyowasiliana na wenzako

**Soma na igiza mazungumzo kati ya Sungura na Chui, kisha jibu maswali yanayofuata.**





FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI DARASA 3.indd 11 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sungura** Habari za leo kaka Chui.

**Chui** Nzuri!

**Sungura** Leo umekunywa maji?

**Chui** Hapana! Sijanywa.

**Sungura** Ooh! Itabidi **nimuagize Pweza** atuletee maji kutoka baharini. Leo bahari ni **shwari**.

**Chui** Hapana! Kuna binadamu anayeitwa Ng'wale anauza maji.

**Sungura** Inaonekana humpendi Pweza.

**Chui** Si kweli! Sina u**adui** na Pweza. Ila maji ya baharini si safi kwa kunywa.

**Sungura** Nina**fikiri** tuwaache wote. Tuagize maji kutoka kwa Kyando.

**Chui** Nina**kubali**ana na wewe. Maji anayouza Kyando ni safi sana.

**Sungura** Kweli! Itabidi tununue hayo.

**Chui** Sawa mdogo wangu.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Sungura anamwitaje Chui?
2. Chui anamwitaje Sungura?
3. Chui alikunywa maji kutoka kwa nani? Kwa nini?
4. Kwa nini Chui alikataa kunywa maji kutoka baharini?
5. Umejifunza nini kutokana na mazungumzo haya?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 12 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana za maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano: kubali** - *kitendo cha kuridhia au kuafiki*

Bibi alikubali kutusimulia hadithi baada ya chakula cha jioni.

Mwalimu alikubali kwenda kuwasalimu wazazi wetu.

1. agiza
2. pweza
3. shwari
4. adui
5. fikiri
6. kubali

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Tazama picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. |  |  |
| 2. |  |  |
| 3. |  |  |
| 4. |  |  |
| 5. |  |  |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) Taja mahali vinapopatikana vitu katika picha namba 1 hadi 5

**Mfano:** Namba 4 machungwa yanapatikana sokoni.

(ii) Taja majina ya vitu hivyo katika umoja na wingi.

**Mfano: kiti – viti**

(iii) Eleza matumizi ya vitu vilivyopo katika picha namba 1 hadi 5.

**Mfano:** Kiti hutumika kukalia.

**B. Jibu maswali yafuatayo:**

(i) Taja vitu vitano vinavyopatikana shuleni.

(ii) Taja majina ya vitu hivyo katika umoja na wingi.

(iii) Eleza matumizi ya kila kimoja.

**C. Andika wingi wa vitu hivi.**

| | | |
|---|---|---|
| (i) gari | (ii) simu | (iii) taa |
| (iv) mti | (v) wembe | (vi) koti |
| (vii) chupa | (viii) mchanga | (ix) nyumba |
| (x) gauni | (xi) nywele | (xii) jiwe |
| (xiii) shati | (xiv) sufuria | (xv) jembe |

**D. Andika umoja wa vitu hivi.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) mayai | (ii) mito | (iii) mifuko | (iv) mabegi |
| (v) maini | (vi) maembe | (vii) miguu | (viii) macho |
| (ix) mabega | (x) vidole | (xi) maji | (xii) unga |
| (xiii) karatasi | | | |

**E. Badili sentensi zifuatazo ziwe katika wingi.**

**Mfano:** Rangi hii ni nzuri.

*Rangi hizi ni nzuri.*

Penseli hii imevunjika.

*Penseli hizi zimevunjika.*



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) Mfuko huu ni mkubwa.
(ii) Meza hii ni safi.
(iii) Nyumba hii ni nzuri.
(iv) Kitabu hiki ni kidogo.
(v) Jiwe hili ni kubwa.

**F. Badili sentensi zifuatazo ziwe katika umoja.**

**Mfano:** Furaha amepewa zawadi ya madaftari.
*Furaha amepewa zawadi ya daftari.*

Walimu wanafundisha vizuri.
*Mwalimu anafundisha vizuri.*

(i) Miti mirefu imeanguka.
(ii) Baba amenunua magari mawili.
(iii) Wanafunzi wamepanda maua mazuri.
(iv) Madarasa yetu yana madirisha makubwa.
(v) Taa za shule yetu zinawaka vizuri.

## Kazi ya Kufanya

**Sikiliza hadithi za watoto kwenye vyanzo mbalimbali vya TEHAMA, kisha isimulie kwa maneno yako mwenyewe.**

## Zoezi la 4: Utungaji

1. Andika hadithi fupi yenye maneno hamsini (50) kuhusu mnyama twiga.
2. Soma kwa sauti hadithi uliyoiandika.
3. Hadithi uliyoiandika inatufundisha nini?

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 15 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Kutumia msamiati

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kutumia msamiati unaohusiana na shughuli zinazofanyika katika maisha ya kila siku. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuelezea shughuli hizo kwa kutumia msamiati unaohusiana na maisha ya kila siku. Pia, utaweza kujieleza kwa kujiamini.*

### Fikiri

Shughuli unazozifanya kila siku unapokuwa shuleni

### Ufahamu

**Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**

### Basi la Lipayo

Sisi tunaishi katika kijiji cha Dingalo. Hapa kijijini basi huondoka na kurudi kila siku. Basi hilo linaitwa Lipayo. Lipayo huanza safari zake kila siku alfajiri. Wasafiri hulisubiri basi kituoni. Likikaribia kituoni, hupiga **honi** kwa nguvu. Wale wanaochelewa hukimbia ili kuliwahi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




Watu hukaa kwenye viti mapema, kisha basi huondoka kuelekea mjini. Basi linapo**fika** mjini, watu wote hu**shuka** na kuelekea kwenye shughuli zao. **Dereva** hupeleka basi kwenye kituo cha mafuta na hujaza mafuta. Baada ya kujaza mafuta, hulirudisha kituoni. Watu wanaoenda kijijini huanza kupanda kwenye basi. **Kondakta** huingia na hupokea **nauli**, kisha hutoa **tiketi**.

Ikifika saa nane, Lipayo huanza safari ya kurudi kijijini. Hubeba mizigo mingi ya madukani na mingine ya **abiria**. Lipayo linapofika karibu na **kituo** cha kwetu, hupiga honi. Watu wengi huenda barabarani kupokea wageni wao. Wengine huenda kupokea mizigo yao iliyoletwa na basi. Tukifunga shule, mimi na dada tutasafiri kwa Lipayo kwenda mjini kumsalimia kaka.



KISWAHILI DARASA 3.indd 17 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Basi linalotoka Dingalo linaitwaje?
2. Basi hilo husafiri siku zipi?
3. Lipayo likikaribia kituoni hufanya nini?
4. Kwa nini Lipayo huondoka mapema sana kijijini?
5. Kazi za kondakta katika basi ni zipi?
6. Wewe umewahi kusafiri kwa basi? Ulienda wapi?
7. Uliona nini njiani?

**Andika NDIYO kwenye sentensi ya kweli na HAPANA kwenye sentensi isiyo ya kweli.**

8. Basi la Lipayo hutoka kijijini mchana.______________
9. Basi linapofika mjini, watu wote hushuka kuelekea kwenye shughuli zao. ______________
10. Basi likifika kituoni kondakta huwaita wasafiri. ______________
11. Basi likitoka kijijini linakuwa tupu.______________
12. Basi la Lipayo hujaza abiria kila siku. ______________

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana za maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano: honi** - *kifaa kwenye chombo cha usafiri ambacho kikibonyezwa/kuvutwa hutoa mlio wa tahadhari kwa watu au vyombo vingine*

*Mimi ninapenda honi ya treni.*

*Dereva alinipigia honi nilipokuwa ninavuka barabara.*

| | | |
|---|---|---|
| 1. honi | 4. dereva | 7. tiketi |
| 2. fika | 5. kondakta | 8. abiria |
| 3. shuka | 6. nauli | 9. kituo |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.**

(i) Mama huchemsha chai kila siku asubuhi.
(ii) Shangazi husoma kitabu cha hadithi kila siku jioni.
(iii) Kaka huosha vyombo mara kwa mara.
(iv) Mimi husoma kitabu kila siku jioni.
(v) Mjomba hupenda kuvaa nguo nyekundu kila mara.
(vi) Bibi hutusimulia hadithi kila siku usiku.
(vii) Dada hufanya mazoezi kila siku asubuhi.
(viii) Sisi husafisha mazingira ya nyumbani kwetu kila wiki.
(ix) Kila Alhamisi, Faraja huvaa nguo za michezo.
(x) Mtoto huyu hulia kila mara.

**B. Jibu maswali haya.**

(i) Huwa unafanya nini kila siku asubuhi?
(ii) Eleza shughuli unazofanya kila Jumamosi.
(iii) Wazazi au walezi wako hufanya nini kila Jumamosi?

**C. Tunga sentensi sita sahihi kwa kutumia jedwali lifuatalo:**

| Kifungu A | Kifungu B | Kifungu C |
|---|---|---|
| Kila siku mwalimu<br>Kila mara dada<br>Kila jioni kaka | hucheza<br>hufundisha<br>hufanya | mazoezi ya viungo<br>wanafunzi darasani<br>mpira wa miguu |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 19 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Panga sentensi hizi kwa mtiririko sahihi ili kupata habari.**

(i) Hutandika vitanda vyao, huoga na kuvaa sare za shule.
(ii) Hunywa chai na kwenda shuleni.
(iii) Husimama mstarini na kuingia darasani.
(iv) Huamka mapema kila siku asubuhi.
(v) Baada ya masomo hurudi nyumbani.
(vi) Hufagia darasa lao na uwanja wa shule.
(vii) Jamali, Hamisi na Rehema wanasoma Darasa la Tatu.

## Zoezi la 4: Miundo

**Tunga sentensi tatu kwa kila muundo.**

1. ... hu_ ...
2. ... mara kwa mara ...
3. ... kila ...

## Kazi ya Kufanya

**Andika shughuli za kila siku zinazofanywa na watu unaoishi nao nyumbani kwenu.**

## Zoezi la 5: Utungaji

**Tunga habari fupi kuhusu shughuli unazozifanya kila siku.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Visawe na vinyume

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kutumia maneno yenye maana sawa ambayo huitwa visawe. Vilevile, utajifunza vinyume vya maneno; yaani maneno yanayopingana na mengine. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia visawe na vinyume katika mazungumzo yako ya kila siku.*

### Fikiri

**Tofauti iliyopo katika maneno yafuatayo:**

1. shangilia - furahia
2. adabu - heshima
3. mfupi - mrefu
4. simama - kaa

### Ufahamu

**Soma hadithi hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**

### Ndovu na Mbogo

Hapo zama za kale, palikuwa na marafiki wawili. Marafiki hao ni **Ndovu** na **Mbogo**. Marafiki hao walipendana sana. Walishirikiana katika shughuli zao za kila siku. Siku moja, Ndovu alipanga safari ya kumtembelea **nyanya** yake kijiji cha jirani. Ndovu alikwenda **gulioni** na kumnunulia nyanya yake zawadi. Zawadi hiyo ilikuwa ni **dagaa** na **jamvi**. Mbogo naye alimchumia maembe Ndovu kwa ajili ya zawadi. Siku ya safari,

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 21 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

marafiki hao wawili waliamka mapema. Walisaidiana kubeba na kuweka vitu kwenye **motokaa**. Mbogo alilazimika kubaki ili kulinda mazao yao yasiharibiwe na **tumbili**. Ndovu alipofika kijijini alikuta nyanya yake amepika **ubwabwa** na mboga za majani. Ndovu na nyanya yake waliketi juu ya jamvi na kula kwa pamoja. Ilipofika jioni Ndovu alifunga safari kurudi kijijini kwake. Nyanya alimpa zawadi ya **peremende**. Ndovu alifurahi sana.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Nani walikuwa marafiki?
2. Andika maneno yenye maana sawa na maneno yaliyokozwa wino katika hadithi uliyosoma.

## Zoezi la pili: Msamiati

**Oanisha maneno na maana zake.**

**Mfano:** jokofu - (b) chombo mfano wa kabati kinachotoa baridi na hutumika kuhifadhia vyakula

| Maneno | Maana |
|---|---|
| 1. jokofu | (a) ada ya shule |
| 2. maliwato | (b) chombo mfano wa kabati kinachotoa baridi na hutumika kuhifadhia vyakula |
| 3. karo | (c) sehemu maalumu ya kujisaidia, kuoga na kujiweka katika hali ya unadhifu |
| 4. gulio | (d) mahali penye mkusanyiko wa wauzaji na wanunuzi wa bidhaa za rejareja |
| 5. peni | (e) malipo ya gari |
| 6. konde | (f) sehemu kubwa ya ardhi iliyolimwa |
| | (g) kalamu ya wino |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 22 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Soma kwa sauti sentensi zenye maneno yenye maana sawa.**

(i)



Hili ni **gari**. Jina lingine huitwa **motokaa**.

(ii)



Huyu ni **tembo**. Jina lingine huitwa **ndovu**.

(iii)



Hizi ni **pipi**. Hupendwa sana na watoto. Vilevile, huitwa **peremende**.

(iv)







Hizi ni **hela**. Jina lingine huitwa **pesa** au **fedha**. Hutumika kununulia vitu mbalimbali.

(v)



Hii ni **kalamu**. Pia, huitwa **peni**. Peni ni kalamu ya wino.

(vi)



Kijana huyu **anakwea** mnazi. Hii ni sawa na kusema **anapanda** mnazi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Chagua maneno yenye maana sawa na kuyaweka pamoja.**

**Mfano:** chumvi – munyu

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (i) chumvi | (ii) muda | (iii) ndala | (iv) tisa | (v) wiki |
| (vi) kandambili | (vii) wakati | (viii) kenda | (ix) munyu | (x) juma |

**C. Oanisha maneno ya sehemu A na B yenye maana sawa.**

**Mfano:** (i) ada - (f) karo

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| (i) ada | (a) jokofu |
| (ii) tamati | (b) maliwato |
| (iii) bafu | (c) keti |
| (iv) friji | (d) dhiki |
| (v) shamba | (e) konde |
| (vi) kaa | (f) karo |
| (vii) shida | (g) mwisho |

**D. Andika majina mawili yenye maana sawa na picha hizi.**

| | | |
|---|---|---|
| **Mfano** (i) |  | treni garimoshi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | | |
|---|---|---|
| (ii) |  | |
| (iii) |  | |
| (iv) |  | |
| (v) |  | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**E. Andika maneno yenye maana sawa na maneno haya.**

(i) mwisho ____________

(ii) faulu ____________

(iii) ona ____________

(iv) waza ____________

(v) beseni ____________

**F. Andika sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yenye maana sawa na yaliyokozwa wino.**

**Mfano:** Kaka **alipanda** kwenye mti mrefu.
Kaka **alikwea** kwenye mti mrefu.

(i) Wanafunzi wote waliambiwa **wakae** kwenye viti.

(ii) Wakulima wa Mkoa wa Tanga wanalima **katani**.

(iii) Tunasherehekea **sikukuu** ya uhuru kila mwaka.

(iv) **Paka** wetu ana rangi nzuri.

(v) Darasa letu lina ma**dawati** mengi.

**G. Tazama picha zifuatazo, kisha andika sentensi yenye neno na kinyume chake.**

**Mfano:** Mwanafunzi anatembea. - Mwanafunzi anakimbia.



tembea



kimbia

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i)



(ii)



(iii)



(iv)



FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 27 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v)





**H. Oanisha maneno ya sehemu A na kinyume chake katika sehemu B.**

**Mfano:** mbali - (e)

| Sehemu A | | Sehemu B |
|---|---|---|
| (i) mbali | ( ) | (a) sahau |
| (ii) maskini | ( ) | (b) lala |
| (iii) kumbuka | ( ) | (c) zibua |
| (iv) amka | ( ) | (d) tajiri |
| (v) ziba | ( ) | (e) karibu |

**I. Chagua neno ambalo ni kinyume kutoka katika orodha hii, kisha jaza nafasi iliyowachwa wazi.**

| |
|---|
| juu, mbaya, adui, lia, bomoa, mwembamba |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| (i) mnene | ____________ |
| (ii) rafiki | ____________ |
| (iii) cheka | ____________ |
| (iv) jenga | ____________ |
| (v) chini | ____________ |
| (vi) mzuri | ____________ |

**J. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:**

| | |
|---|---|
| (i) ingia | ____________ |
| (ii) ____________ | sahau |
| (iii) kidogo | ____________ |
| (iv) ____________ | rudi |
| (v) kusanya | ____________ |
| (vi) polepole | ____________ |

**K. Andika kinyume cha maneno yaliyokozwa wino katika sentensi hizi.**

(i) Baba alipanda kwenye gari **dogo**.

(ii) Limbi anasoma shule iliyopo **mbali**.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Kitanda changu ni **kifupi**.
(iv) Wavuvi walivua samaki **wakubwa**.
(v) Bibi alivuna mahindi **machache**.

## Kazi ya kufanya

**Soma vitabu kutoka maktabani au katika vyanzo mbalimbali vya TEHAMA, kisha fanya yafuatayo:**

1. Andika maneno kumi na visawe vyake.
2. Andika maneno kumi na vinyume vyake.

## Zoezi la 4: Utungaji

**Soma hadithi hii, kisha fanya zoezi linalofuata.**

### Mfalme mjinga

Siku moja mfalme **mjinga** aliitisha mkutano. Wananchi wake walikusanyika kwa wakati uliopangwa. Katika mkutano huo, aliwataka wananchi wake kufanya mambo yao kwa ushirikiano. Aliwataka **maskini** wote wawasaidie wasiojiweza. Vilevile, aliamuru **kuvunjwa** kwa nyumba za kisasa. Mfalme mjinga aliwakumbusha wananchi wake **kupunguza** vyumba vya madarasa. Halafu, aliwahimiza wananchi wake **kung'oa** miti mbalimbali katika mazingira yao. Wananchi wote **walikasirika**, hivyo hawakuonesha ishara ya kumuunga mkono.

### Zoezi

Rudia kuandika hadithi hii kwa kuandika kinyume cha maneno yaliyokozwa. Kichwa cha hadithi kiwe MFALME MWEREVU.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Methali, nahau na vitendawili

### *Utangulizi*

*Katika sura hii, utajifunza methali, nahau na vitendawili. Utaweza kuanzisha na kumalizia methali. Vilevile, utaweza kueleza maana zake. Pia, utaweza kufahamu maana na matumizi ya nahau. Halikadhalika, utaweza kutega na kutegua vitendawili kwa kuvihusisha na mazingira yanayokuzunguka. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuwasiliana katika miktadha mbalimbali.*

**Fikiri**

Tofauti zilizopo katika sentensi zifuatazo:

1. Asiyefunzwa na mamaye, hufunzwa na ulimwengu.
2. Ana mkono wa birika.
3. Kuku wangu ametagia mibani.

**Ufahamu**

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Rushwa ni adui wa haki**

Siku moja, Mtendaji wa Kata ya Kadwiga aliitisha mkutano katika ofisi ya Kata. Kata hiyo ina vijiji vitano ambavyo ni Muungano, Ujamaa, Mapinduzi, Azimio na Mtakuja. Wanakijiji kutoka vijiji hivyo walihudhuria kwa wingi. Viongozi kutoka vitongoji mbalimbali nao walihudhuria. Mtendaji alifungua mkutano kwa kueleza kuwa lengo kuu la mkutano huo ni kujadili mbinu za ku**tokomeza**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 31 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

vitendo viovu vilivyo**kithiri** katika kata hiyo. Mtendaji alianza kikao hicho kwa kuwakaribisha watu wote na kuwaomba watoe ushirikiano na michango mbalimbali. Mtendaji aliendelea kusema kuwa tunatakiwa tuwe kitu kimoja ili kupambana na **maovu** hayo kwani kidole kimoja hakivunji chawa.

Baada ya ufunguzi huo, Mtendaji wa Kata alianza kikao kwa kusema kuwa vitendo vya rushwa vimekithiri katika Kata ya Kadwiga. Mtendaji aliendelea kwa kusema kuwa vitendo vya rushwa vimepoteza haki za raia wema. Pia, vijana wengi wamekuwa na mkono mrefu, watoto wanabakwa, wanawake wengi wanapigwa na waume zao. Vilevile, watoto wa kike na wa kiume wanakatishwa masomo na wengine wanalawitiwa. Halikadhalika, vitendo vya wizi na ujambazi vimeongezeka na kuleta madhara makubwa. Watoto wengine na vijana wanavuta bangi na kutumia dawa za kulevya. Haya yote yanafumbiwa macho kwa sababu ya kupokea na kutoa mlungula.

Alipomaliza kusema hayo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mtakuja alimsifu kwa kuona madhara yatokanayo na rushwa. Kiongozi wa Kikosi cha Sungusungu naye kwa ukakamavu alisimama na kusema kuwa anaomba **ridhaa** ya wajumbe ili awashughulikie watu wote wenye mkono mrefu. Kiongozi huyu aliendelea kwa kusema kuwa ndege mjanja hunaswa kwenye tundu bovu. Kama maovu yataendelea, yeyote atakayekamatwa atakiona cha mtema kuni. Alihitimisha hoja yake kwa kusema kuwa wanakijiji wanatakiwa kuchukua hatua kali dhidi ya vitendo vyote viovu kwani usipoziba ufa utajenga ukuta.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwakilishi wa kikundi cha wanawake katika Kata ya Kadwiga, Mama Doto alisema kuwa hawapendi kuona watoto wao wanaharibika kwa kuwa kila mchuma **janga** hula na wa kwao. Mama Doto na wanawake wenzake waliwaomba viongozi kuchukua hatua kali kwa yeyote atakayethibitika kutenda kosa na atakayekula mlungula.

Baada ya hayo yote, Mtendaji wa Kata alifunga kikao kwa kusema kuwa kila mwananchi anatakiwa kuishi kwa kuzingatia kanuni na sheria zilizowekwa ili kutenda matendo mema na kuleta maendeleo ya taifa kwa ujumla.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Taja maovu yanayotendeka katika Kata ya Kadwiga.
2. Taja methali zilizopo kwenye habari hii.
3. Eleza maana ya nahau zilizopo katika habari hii.
4. Taja vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu vilivyopo katika Kata ya Kadwiga.
5. Madhara ya rushwa yanatokea kwa kasi kubwa kwa sababu gani?
6. Umejifunza nini kutokana na habari hii?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana za maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano: maovu** - matendo mabaya

*Viongozi wetu wametuonya tusitende maovu.*

*Wazazi wote hawapendi matendo maovu.*

1. tokomeza
2. kithiri
3. maovu
4. ridhaa
5. janga

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3: Methali

**A. Anzisha na malizia methali zifuatazo kwa kuchagua jibu sahihi kwenye kisanduku.**

| |
|---|
| hajikwai, samaki mkunje, asiyefunzwa na mamaye, yaumiza matumbo, hula mbivu, siku za mwizi, haina baraka, kuuliza, umoja ni nguvu, haiozi, yaumiza matumbo, mtoto umleavyo, hakivunji chawa |

**Mfano:** Ngojangoja ..................

Ngojangoja <u>yaumiza matumbo.</u>

.................. ndivyo akuavyo.

<u>Mtoto umleavyo</u> ndivyo akuavyo.

(i) Mvumilivu ..................

(ii) .................. si ujinga.

(iii) Mwenda pole ..................

(iv) .................. ni arobaini.

(v) Akiba ..................

(vi) .................. utengano ni udhaifu.

(vii) Haraka haraka ..................

(viii) .................. angali mbichi.

(ix) Kidole kimoja ..................

(x) .................. hufunzwa na ulimwengu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Soma na igiza mazungumzo yafuatayo na wenzako.**

1.



Mimi ni Bomba. Ninatoa maji ambayo yana matumizi mengi. Ninajua methali isemayo **ndondondo si chururu**.

2.



Mimi ni Ndoo. Ninaweza kuwekewa maji mengi. Ninajua methali isemayo **maji yakimwagika hayazoleki**.

3.



Sisi ni Nyuki. Tunaishi kwenye mzinga. Tunatengeneza asali tamu sana. Tunajua methali isemayo **fuata nyuki ule asali** lakini ukituchokoza tunakuuma.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4.



Mimi ni Nyegere. Ni mnyama mdogo. Ninapenda sana kula asali. Ninajua maana ya methali fuata nyuki ule asali. Maana yake ni kuwa **fuata wema upate mema**. Mimi hutembelea maeneo yenye asali. Ushuzi wangu huwalevya nyuki.

5.



Mimi ni Sungura. Ni mnyama mjanja kuliko wote. Daima nina haraka sana. Ninajua methali isemayo **haraka haraka haina baraka**.

6.



Mimi ni Fisi. Ni bwana afya wa porini. Ninajua maana ya methali isemayo asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Maana yake ni kuwa **asiyesikia anayoambiwa na wakubwa mwisho hupata matatizo**. Kutokana na uroho wangu mara nyingi napata matatizo makubwa.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 36 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kwanza ya kufanya

**Soma vitabu kutoka vyanzo mbalimbali vya TEHAMA au maktabani, kisha andika methali kumi na maana zake.**

## Zoezi la 4: Nahau

**Toa maana ya nahau zilizopigiwa mstari kwa kuchagua jibu sahihi kwenye kisanduku.**

| |
|---|
| (i) ni mchoyo (ii) ni mwizi (iii) ameoa (iv) amelewa |
| (v) kwa kushirikiana (vi) kufa moyo (vii) kukubaliana (viii) amua |

**Mfano:**

Baada ya kusubiri kwa muda mrefu <u>alikata shauri</u> kuondoka.
Kata shauri maana yake ni <u>amua</u>.

(i) Kaka <u>amepata jiko.</u>
(ii) Mjomba <u>amevaa miwani.</u>
(iii) Juma ana <u>mkono mrefu.</u>
(iv) Wanakijiji wanafanya kazi <u>bega kwa bega.</u>
(v) Chausiku ana <u>mkono wa birika</u>.

## Kazi ya pili ya kufanya

**Tafuta nahau kumi na maana zake kutoka katika vyanzo mbalimbali vya TEHAMA au maktabani.**

## Zoezi la 5: Vitendawili

**A. Oanisha vitendawili vilivyopo sehemu A na picha zinazotegua vitendawili hivyo katika sehemu B, kisha andika jina la picha kwenye nafasi iliyoachwa wazi.**

| Na. | Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|---|
| (i) | Kuku wangu katagia mibani. ______ |  |



FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI DARASA 3.indd 37 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | | |
|---|---|---|
| (ii) | Nyumba yangu ina nguzo moja. _______ |  |
| (iii) | Babu kalala ndevu nje. _______ |  |
| (iv) | Nyumba yangu haina mlango. _______ |  |
| (v) | Mtoto wangu nikimpa chakula analia nisipompa ananyamaza. _______ |  |
| (vi) | Juu mboga katikati kuni chini ugali. _______ |  |
| (vii) | Tajiri wa rangi. _______ |  |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Tega na tegua vitendawili vifuatavyo kwa kuchagua jibu sahihi.**

| |
|---|
| machicha ya nazi, ajenga ingawa hana mikono, matairi ya gari, mbwa, kitanda, kinywa, popoo mbili zavuka mto, anga na nyota, firigisi, kivuli, ni rafiki na ni adui |

(i) Koti la babu halikosi chawa. ..................

(ii) Kisima cha bibi hakikauki. .................

(iii) Ngozi ndani nyama juu. ..................

(iv) Kila niendako ananifuata. ..................

(v) ........................................................ macho

(vi) ........................................................ moto

(vii) Nyanya yako ana huruma hukubeba ulalapo. ..................

(viii) ................................................. ndege

**C. Tegua vitendawili vifuatavyo kwa kutumia picha "a" hadi "f", kisha andika herufi ya jibu sahihi kwenye nafasi zilizoachwa wazi.**

(i) Ukoo wetu hauishiwi na safari. _______

(ii) Kafa huku akining'inia. _______

(iii) Mwanangu hunipa kitu kitamu lakini akichokozwa hutawanya watu. _______

(iv) Ana miguu ya msumeno. _______

(v) Anakula lakini hashibi. _______

(vi) Ana mdomo lakini anauma kwa mkia. _______

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(a)


(b)


(c)


(d)


(e)


(f)


**D. Andika majibu ya vitendawili hivi.**

(i) Anajua kuchora ingawa hajui anachokichora. ______

(ii) Rafiki yangu ni mharibifu lakini ninamuhitaji. ______

(iii) Anabeba mishale kila anapokwenda. ______

(iv) Wazee wawili wanashuka mlima. ______

(v) Anafundisha kutengeneza mwavuli. ______

## Kazi ya tatu ya kufanya

**Sikiliza vipindi mbalimbali vya watoto kutoka kwenye vyombo vya habari, kisha andika vitendawili kumi na majibu yake.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 6: Utungaji

**Soma habari ifuatayo, kisha jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika methali, nahau na vitendawili vilivyopo kwenye boksi.**

| |
|---|
| asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu, mchuma janga hula na wa kwao, miaka nenda miaka rudi, hakufua dafu, siku za mwizi ni arobaini, kupiga maji, sikio la kufa halisikii dawa, mkono mrefu, kukata mzizi wa fitina |

### Madhara ya dawa za kulevya

Chaupele ni kijana mkorofi sana anayependa kuvuta bangi. Vilevile, ana 1.________na anapenda 2.____________hadi kuanguka mtaroni. Ndugu zake wamekuwa wakimuonya kuacha tabia hizo 3.__________ lakini Chaupele hasikii kwani 4.___________. Siku moja alivuta bangi sana, kisha akaenda kijiji cha jirani kuiba baiskeli ya balozi. Baada ya tukio hilo, aliona vijana wanne wakimkimbiza na kumwambia atupe baiskeli chini. Ama kweli 5.____________, hakutegemea kuwa angekamatwa. Alijitahidi kuongeza mwendo lakini 6.____________. Vijana hao walimpiga sana kwa sababu walikuwa na hasira kali. Vilevile, walitaka 7.____________ kwa kumchoma moto. Ghafla, akatokea mzee mmoja mwenye hekima na busara hapo kijijini akawakataza vijana hao wasimuue. Mzee huyo alishauri Chaupele apelekwe polisi. Baadaye alipelekwa mahakamani na aliamriwa alipe faini ya shilingi laki tatu na arudishe baiskeli hiyo.

Chaupele hakuwa na hiyo fedha. Ndugu zake walichangishana ili hiyo pesa ipatikane kwani 8.____________. Baada ya kulipa fedha hiyo, ndugu zake walimuonya kwa mara ya mwisho. Walimtahadharisha kuwa atakuja kupatwa na matatizo makubwa kwani 9.____________.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Alama za uandishi

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza matumizi ya alama za uandishi. Pia, utajifunza matumizi ya viunganishi vya ushikamani na vihusishi katika habari. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia alama za uandishi, viunganishi vya ushikamani na vihusishi katika matini. Aidha, utaweza kufanya uhariri wa kazi za wenzako katika matini sahili.*

### Fikiri

1. Kitu kinachokufanya upumzike unaposoma sentensi.
2. Kitu kinachokufanya upumzike kidogo unaposoma sentensi.
3. Kitu kinachokufanya uelewe kama unaulizwa swali.

**Ufahamu**

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Kituo cha afya**

Mimi ninaitwa Luka. Kaka yangu anaitwa Kizenga. Tunaishi katika Kijiji cha Kwale. Mbele ya nyumba yetu kuna kituo cha **afya**. Siku moja niliugua mafua makali na kikohozi. Baba aliniuliza, "Umeanza lini kukohoa?" Nilimjibu, "Nilianza kukohoa tangu jana jioni." Baba alimwambia kaka, "Kizenga mpeleke Luka kwenye kituo cha afya akatibiwe." Hata hivyo, kaka aliponiona ali**shangaa** akasema, "Lo! Kumbe unaumwa sana? Pole sana mdogo wangu. Twende kwenye kituo cha afya ukatibiwe."

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




Tulipofika kwenye kituo cha afya, nilijiandikisha kumuona daktari. Baada ya muda, **muuguzi** alikuja akasimama mbele ya wagonjwa na kuita majina. Aliita jina langu na kutupeleka katika chumba cha daktari. Mimi na kaka tuliingia kwa daktari. Tulipofika kwa daktari, nilimueleza jinsi ninavyo**umwa**. Daktari aliniuliza, "Ulianza kukohoa lini?" Nilimjibu, "Nilianza kukohoa jana jioni." Daktari alinielekeza niende maabara kupima. Majibu yalipotoka, daktari aliniandikia dawa. Baada ya kupata **matibabu**, mimi na kaka tulirudi nyumbani. Hali yangu iliendelea kuwa nzuri na watu wote walifurahi.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Taja alama za uandishi zilizojitokeza katika habari hii.
2. Alama gani za uandishi zimejitokeza mara nyingi zaidi?
3. Taja maneno yanayounganisha mawazo kwenye habari hii.



KISWAHILI DARASA 3.indd 43 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana za maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano:** **umwa** - *pata au hisi maumivu au dhoofika mwili kutokana na ugonjwa au dalili zake*
*Dada alipoumwa homa kali aliwahishwa hospitalini.*
*Jumanne aliumwa malaria kwa kuwa alikuwa hatumii chandarua.*

1. afya
2. shangaa
3. muuguzi
4. umwa
5. matibabu

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Andika NDIYO kwenye sentensi ya kweli au HAPANA kwenye sentensi isiyo ya kweli.**

(i) Vilevile, timu yetu ilifunga magoli mawili. Neno **vilevile** ni jina la timu. ____________

(ii) Alama ya mkato ni hii (**?**). ____________

(iii) Alama ya nukta ni hii (**.**). ____________

(iv) Mwalimu amesimama mbele ya darasa. Neno **mbele** linaonesha mahali aliposimama mwalimu. ____________

(v) Alama ya mkato ni hii (**,**). ____________

(vi) Alama ya mshangao ni hii (**!**). ____________

(vii) Hata hivyo, tulimpigia makofi matatu. **Hata hivyo** si kiunganishi. ____________

(viii) Misheli amesimama kando ya mto. Neno **kando** maana yake ni mbali. ____________

**B. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi. Hakikisha unaweka alama sahihi za uandishi na herufi kubwa**.

(i) sebo anaishi mkoa wa morogoro

(ii) wanafunzi walitembelea mbuga za wanyama za mikumi serengeti na ruaha



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) lo mtoto ameanguka

(iv) shambani kwenu kuna mazao gani

**C. Tazama picha zifuatazo, kisha jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyopo kwenye kiboksi.**

| |
|---|
| nyuma, mbele, juu, kando, kushoto, chini, katikati, pembeni, ndani, kulia |

(i)



Mpira upo _____ ya kiti.

(ii)



Begi lipo _____ ya meza.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii)



Msichana amesimama _____ ya ndoo.

(iv)



Kikombe kipo _____ ya kabati.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 46 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Upendo yupo upande wa _____ wa Hamisi.

(vi) Hamisi yupo upande wa _____ wa Upendo.



(vii) Basi lipo _____ ya lori.



FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 47 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(viii) Ng'ombe yupo _____ ya mbuzi.



(ix) Mtoto anatembea _____ ya barabara.



(x) Mtoto amesimama _____ ya wazazi.





KISWAHILI DARASA 3.indd 48 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Soma habari hii, kisha fanya zoezi.**



Amosi alikuwa **juu** ya mti akichuma maembe. Mti wa maembe ulikuwa **kando** ya nyumba yao. Mti huo ulikuwa na maembe mengi sana. Ulikuwa na maembe mabichi na yaliyoiva. Amosi alichuma maembe yaliyoiva na kuyadondosha chini. Lulu na Kiba walimsaidia kuokota maembe na kuyatia **ndani** ya ndoo. Walipomaliza kuokota maembe yaliyokuwa **chini** ya mti, waliingia nayo ndani. Walipofika ndani, waliyaosha na kuyapanga **ndani** ya jokofu.

**Maswali**

(i) Amosi alikuwa ______ ya mti akichuma maembe.
(ii) Mti wa maembe ulikuwa ______ ya nyumba.
(iii) Lulu na Kiba waliyatia maembe ______ ya ndoo.

**E. Andika NDIYO kwenye sentensi ya kweli na HAPANA kwenye sentensi isiyo ya kweli.**

(i) Ndege hukaa juu ya mti.______________
(ii) Wanafunzi hukaa chini ya viti. ______________
(iii) Maua hupandwa kando ya nyumba. ______________
(iv) Ng'ombe huishi ndani ya maji. ______________
(v) Binadamu huishi ndani ya nyumba. ______________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## F. Soma na igiza

(i)



Mimi ni **nukta**. Ninatumika mwishoni mwa sentensi. Alama yangu ni hii **.**

(ii)



Mimi ni **mkato**. Watu wengi huniita kituo kidogo. Ninatumika kutenganisha vitu vilivyoorodheshwa kwa mfululizo na kuweka pumziko dogo. Alama yangu ni hii**,**

(iii)



Mimi ni **mshangao.** Watu hunitumia kila wanaposhangaa, wanaposhituka na wanaposisitiza jambo. Alama yangu ni hii **!**

(iv)



Mimi ni **kiulizo**. Ninatumika kila linapoulizwa swali. Alama yangu ni hii **?**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**G. Weka alama ya uandishi mbele ya jina la alama.**

**Mfano:** Nukta ______.______

| **Jina** | **Alama** |
|---|---|
| (i) Mkato | ______________ |
| (ii) Mshangao | ______________ |
| (iii) Kiulizo | ______________ |
| (iv) Nukta | ______________ |

**Kazi ya kufanya**

**Kusanya kazi zenye alama za uandishi zifuatazo: nukta, mkato, mshangao na kiulizo, kisha pigia mstari alama hizo.**

**Zoezi la 4: Utungaji**

**Chagua jibu sahihi kwenye kiboksi, kisha jaza nafasi zilizoachwa wazi kwenye kifungu cha habari.**

| vilevile, ingawa, hata hivyo, isipokuwa |
|---|

Amani anaishi na bibi yake katika kijiji cha Kilole. Anamsaidia bibi yake shughuli za nyumbani. ______________, anamsaidia kusafisha nyumba, kupika, kuosha vyombo na kufua. Amani huwa anafanya hivyo kila mara ______________ siku ya Jumamosi tu. Siku hiyo Amani hushinda kwenye michezo mbalimbali ______________ jioni hupika chakula. ______________, Amani hufanya juu chini mpaka aoshe vyombo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Kusikiliza mazungumzo

### *Utangulizi*

*Katika sura hii, utajifunza kusikiliza mazungumzo kwa kuzingatia mambo ya msingi katika miktadha mbalimbali. Aidha, utaweza kutumia maarifa uliyoyasikia katika miktadha mingine ya mazungumzo.*

### Fikiri

1. Hadithi yoyote ambayo uliwahi kusimuliwa.
2. Mambo yaliyokuwemo katika hadithi hiyo.
3. Mafunzo uliyoyapata katika hadithi hiyo.

### Ufahamu

**Sikiliza habari hii ikisomwa, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Kusoma ni haki yetu**

Kayande ni mwanafunzi wa Darasa la Tatu. Anasoma katika **Shule** ya Msingi Juhudi. **Rafiki** yake anaitwa Jema. Mdogo wake Jema anaitwa Furaha. Furaha anasoma Darasa la Pili.

Siku moja, Kayande aliamka mapema ili awahi kwenda shuleni. Alipokuwa njiani, alikutana na rafiki yake Jema pamoja na mdogo wake Furaha. Jema na Furaha walikuwa wana**chunga** ng'ombe. Kayande aliwauliza, "Leo hamuendi shuleni?" Jema alijibu, "Ndiyo

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 52 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hatuendi. Baba ametuambia tukachunge ng'ombe. Yeye anakwenda kwenye mkutano." Kayande aliwaambia, "Si vyema kukosa kwenda shuleni. Kusoma ni **haki** yetu."

Shuleni mwalimu aliita majina. Jina la Jema lilipoitwa, Kayande alijibu, "Amekwenda kuchunga ng'ombe." Mwalimu na wanafunzi wali**sikitika**. Mwalimu akasema, "Mwanafunzi asipofika shuleni anakosa haki yake ya kupata elimu na atakuwa **mjinga**." Mwanafunzi mmoja alimuuliza mwalimu, "Haki za mtoto ni zipi?" Mwalimu akajibu, "Kila mtoto ana haki ya kupata elimu, kupendwa na kusikilizwa." Mwalimu aliendelea kusema kuwa, "Mwanafunzi anapo**hudhuria** masomo shuleni, hujifunza mambo mengi. Pia, ataweza kujiamini na kufanikiwa katika maisha yake."



Mwanafunzi mmoja alimuuliza mwalimu, "Wazazi wakitu**zuia** kuja shuleni tufanye nini?" Mwalimu akajibu, "Mnatakiwa kuwaagiza wenzenu kutoa taarifa hapa shuleni." Kayande alimuuliza tena mwalimu, "Wazazi hao watafanywa nini?" Mwalimu akajibu, "Wataitwa shuleni kujieleza. Aidha, wataelezwa umuhimu wa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuwaruhusu watoto wao kuhudhuria shuleni kila siku." Wanafunzi wote walifurahi kusikia maneno ya mwalimu.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Nani anasoma Darasa la Tatu?
2. Rafiki yake Kayande anaitwa nani?
3. Kwa nini Jema na Furaha hawakwenda shuleni?
4. Mwanafunzi akienda shuleni kila siku atapata faida gani?
5. Watoto wana haki gani?
6. Unatakiwa kufanya nini mzazi au mlezi wako akikuzuia kwenda shuleni?
7. Habari hii inakufundisha nini?

## Zoezi la pili: Msamiati

**A. Oanisha maneno na maana zake.**

**Mfano:**

**shule** - *(g) mahali ambapo wanafunzi hupata elimu*

| Maneno | Maana |
|---|---|
| (i) shule | (a) fanya jambo lisitokee au lisiendelee kufanyika |
| (ii) chunga | (b) peleka mifugo malishoni na kuwalinda wasidhuriwe au kuibwa |
| (iii) haki | (c) mtu asiyejua kitu au jambo fulani |
| (iv) sikitika | (d) pata huzuni kutokana na jambo baya lililotokea |
| (v) mjinga | (e) kitu ambacho mtu anastahili kukipata |
| (vi) hudhuria | (f) fika mahali panapofanyika jambo, kama vile mkutano, sherehe au shule |
| (vii) zuia | (g) mahali ambapo wanafunzi hupata elimu |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano: Rafiki** - *mtu unayempenda na kumuamini*

*Nina marafiki wawili, Erika na Joshua.*

*Dada yangu ana marafiki wengi sana.*

(i) shule
(ii) rafiki
(iii) chunga
(iv) haki
(v) mjinga

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua jibu lililo sahihi.**

(i) Kayande aliamka mapema ili afanye nini?
  (a) Awahi kwenda shule
  (b) Awahi kwenda nyumbani
  (c) Awahi kwenda sokoni
  (d) Awahi kwenda shambani

(ii) Kwa nini Jema na Furaha hawakwenda shule?
  (a) Walikwenda kuchunga mbuzi
  (b) Walikwenda kuchunga kondoo
  (c) Walikwenda kuchunga ng'ombe
  (d) Walikwenda kuchunga punda

(iii) Mwalimu alisema kuwa mwanafunzi asipofika shuleni atakosa nini?
  (a) Haki yake ya kupata chakula
  (b) Haki yake ya kupata mavazi
  (c) Haki yake ya kupata elimu
  (d) Haki yake ya kucheza na wenzake

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Wazazi wakituzuia kuja shuleni tufanye nini?
   (a) Twende shambani kuchunga ng'ombe
   (b) Twende sokoni kuuza mboga
   (c) Tukae nyumbani tulee watoto
   (d) Tutoe taarifa shuleni

(v) Nani aliyewaambia Jema na mdogo wake waende kuchunga ng'ombe?
   (a) Kaka
   (b) Baba
   (c) Dada
   (d) Mama

**B. Andika NDIYO kwenye sentensi ya kweli na HAPANA kwenye sentensi isiyo ya kweli.**

(i) Kayande ni mwanafunzi wa Darasa la Sita.__________

(ii) Furaha anasoma Darasa la Pili. __________

(iii) Kayande anasoma Shule ya Msingi Bidii. __________

(iv) Kila mtoto ana haki ya kusoma, kupendwa na kusikilizwa. __________

(v) Mwanafunzi akisoma kwa bidii atafanikiwa katika maisha yake. __________

## Kazi ya kufanya

**Sikiliza hadithi kutoka vyanzo mbalimbali vya TEHAMA kama vile maktaba mtandao, kisha andika mafunzo uliyoyapata.**

## Zoezi la 4: Utungaji

**Andika habari fupi kuhusu shule yako.**



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Kutumia kamusi

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza maana ya kamusi na jinsi ya kuitumia. Vilevile, utajifunza jinsi maneno na maana zake zinavyoandikwa katika kamusi. Maarifa haya yatakusaidia kutambua mpangilio wa herufi za alfabeti za Kiswahili, kutumia na kutamka maneno ya lugha kwa usahihi katika mawasiliano.*

### Fikiri

Mahali ambapo unapata maana za maneno

**Ufahamu**

**Kusoma mpangilio wa herufi za alfabeti ya Kiswahili.**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| *a* | *b* | *ch* | *d* | *e* | *f* | *g* |
| *h* | *i* | *j* | *k* | *l* | *m* | *n* |
| *o* | *p* | *r* | *s* | *t* | *u* | *v* |
| *w* | *y* | *z* | | | | |

Imba wimbo wa alfabeti ya Kiswahili.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

**A. Jibu maswali yafuatayo:**

(i) Kuna herufi ngapi za alfabeti katika wimbo ulioimba?

(ii) Taja herufi zote za alfabeti kwa mfuatano sahihi kuanzia **a** hadi **z**.

(iii) Taja herufi ya mwanzo katika alfabeti.

(iv) Taja herufi ya mwisho katika alfabeti.

(v) Taja herufi tano za mwanzo kwa mfuatano.

(vi) Taja herufi iliyopo kabla ya **o**.

(vii) Taja herufi inayofuata baada ya **t**.

(viii) Taja herufi iliyopo kati ya **k** na **m**.

**B. Jibu maswali yafuatayo:**

(i) Andika herufi ya kwanza ya jina lako.

(ii) Taja maneno matatu yanayoanza na herufi **m**.

(iii) Taja maneno mawili yanayoanza na herufi **s**.

### Ufahamu

**Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**

### Tutumie kamusi

Siku moja mwalimu wa somo la Kiswahili alisema, "Leo tutajifunza jinsi ya kutafuta maana za maneno kwa kutumia kamusi." Alisema kuwa tutaanza na neno **adabu.** Mwalimu alitupanga katika makundi, kisha alitupatia kamusi moja kila kundi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




Alituambia tufungue ukurasa wa kwanza wenye maneno yanayoanza na herufi **Aa**. Sote tulifungua kamusi. Mwalimu aliendelea kusema, "Tutafute maana ya neno **adabu**."

Mazungumzo yetu yaliendelea hivi.

| | |
|---|---|
| **Mwalimu** | Neno **adabu** linaanza na herufi gani? |
| **Subira** | Neno adabu linaanza na herufi **a**. |
| **Mwalimu** | Vizuri! Herufi ya pili ya neno adabu ni ipi? |
| **Raya** | Herufi ya pili ya neno adabu ni **d**. |
| **Mwalimu** | Uko sahihi! Sasa tuangalie ukurasa wenye maneno yanayoanza na herufi **a** ikifuatiwa na **d**. Ipi ni herufi ya tatu ya neno adabu? |
| **Neema** | Herufi ya tatu ya neno adabu ni **a**. |
| **Mwalimu** | Sawa! Herufi inayofuata ni ipi? |
| **Roda** | Herufi inayofuata ni **b**. |
| **Mwalimu** | Vizuri! Herufi ya mwisho ni ipi? |



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| **Subira** | Herufi ya mwisho ni **u**. |
| **Mwalimu** | Vizuri sana! Je, mmeona neno adabu na maana yake? |
| **Wanafunzi** | Ndiyo mwalimu! |
| **Mwalimu** | Vizuri! Tueleze maana ya neno **adabu** kwa kusoma kutoka kwenye kamusi. |
| **Neema** | Adabu ni tabia njema, nidhamu na heshima; ni mwenendo mwema wa mtu kwake na kwa watu wengine. |
| **Mwalimu** | Vema! Sasa tutafute maana ya neno **mzigo**. Je, neno hilo tutalitafuta kwenye herufi gani? |
| **Roda** | Tutalitafuta kwenye herufi **m**. |
| **Mwalimu** | Vizuri! Fungua kamusi kwenye ukurasa wenye herufi **m**. Herufi ipi inayofuata katika neno mzigo? |
| **Raya** | Ni herufi **z**. |
| **Mwalimu** | Vizuri sana! Herufi nyingine zinazofuata ni zipi? |
| **Joeli** | Ni herufi **i**, **g** na **o**. |
| **Juma** | Mwalimu, tumeshaliona neno **mzigo**. Maana yake ni kitu chochote kinachofungwa na kubebwa. |
| **Mwalimu** | Vizuri sana! Nani anaweza kuniambia kamusi ni nini? |
| **Joeli** | Kamusi ni kitabu chenye maneno yaliyopangwa kwa alfabeti, kinachoeleza maana za maneno. |
| **Mwalimu** | Vizuri sana! Sasa tuendelee kutafuta maana za maneno mbalimbali kwa kutumia kamusi. Maneno hayo ni **mbuga**, **dereva**, **kivuli**, **ghala** na **samani**. Naamini mtatafuta maana ya maneno haya kwa usahihi. |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 60 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la pili: Ufahamu

1. Taja majina ya wahusika waliopo kwenye habari.
2. Utazingatia mambo gani ukitaka kupata neno kwenye kamusi kwa urahisi?
3. Mzazi akikwambia kuwa una adabu, anakuwa ana maana gani?
4. Neno mzigo linapatikana katika kamusi kwenye ukurasa unaoanza na herufi gani?
5. Unajifunza nini kutokana na habari hii?

## Zoezi la 3: Msamiati

**Tumia kamusi kuandika maana za maneno yafuatayo:**

1. mbuga 2. dereva 3. kivuli 4. ghala 5. samani

**Ufahamu**

**Imba shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Kiswahili lugha yetu, tunapaswa kuijua,
Maneno ya lugha yetu, twatakiwa kuyajua,
Ndani ya kamusi yetu, maneno kuangalia,
Kamusi ya Kiswahili, twatakiwa kutumia.

Wanafunzi tujifunze, kamusi kuitumia,
Na herufi tujifunze, vizuri kujisomea,
Vitabuni tujifunze, kamusi kuitumia,
Kamusi tuitumie, na maana kuzijua.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kusoma kwa ufahamu, maneno tunahitaji,
Maneno kuyafahamu, na maana twahitaji,
Ni vema tukafahamu, kamusi twaihitaji,
Kamusi tuzitumie, na maana kuzijua.

Hebu wewe tutajie, neno unalolijua,
Wote tulifikirie, maana kukuambia,
Maana tukuambie, kamusi kuipitia,
Kamusi ya Kiswahili, twatakiwa kutumia.

Herufi zimeandikwa, maneno kutiririka,
Maneno yameandikwa, maana zinasomeka,
Kamusi imeandikwa, maneno yamepangika,
Kamusi ya Kiswahili, twatakiwa kutumia.

Kamusi ya Kiswahili, ni vema tukatumia,
Wote tunastahili, kamusi kuitumia,
Maneno ya Kiswahili, maana tutazijua,
Kamusi ya Kiswahili, twatakiwa kutumia.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 4: Ufahamu

1. Shairi hili linahusu nini?
2. Shairi linasisitiza wanafunzi wafanye nini?
3. Kamusi ina faida gani?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

**A. Panga maneno yafuatayo kialfabeti.**

mama, miti, polisi, mtu, nje, mwalimu, shule, kijiti, kataza, nguo, kijiji, sahani, dada, kituo, ndoo, alfabeti, njano, herufi, maneno, Januari

**B. Panga majina ya marafiki zako kumi kialfabeti.**

## Kazi ya kufanya

**Andika maneno thelathini na maana zake kwa kufuata mpangilio wa alfabeti.**

## Zoezi la 6: Utungaji

**Tunga sentensi nane zenye maneno yanayoanza na herufi B, D, N na M.**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 63 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Kusoma kwa ufahamu na ufasaha

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza mbinu za kusoma kwa ufahamu na ufasaha. Aidha, utaweza kujibu maswali kutokana na habari uliyoisoma. Vilevile, utajifunza namna ya kusoma kwa kasi kwa kufuata alama za uandishi, kupanda na kushuka kwa sauti ya msomaji na lafudhi sahihi ya Kiswahili.*

**Fikiri**

Mambo yanayokuvutia wakati unamsikiliza mtu akisoma.

### Ufahamu

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Mtoto mwema**

Fikiri ni mwanafunzi wa Darasa la Tatu. Anasoma katika Shule ya Msingi Kiegea. Fikiri ana dada mmoja na kaka wawili. Yeye ni **kitindamimba** katika familia yao. Fikiri anaishi na shangazi yake katika Mkoa wa Morogoro. Shangazi yake anaitwa Neema.

Fikiri anampenda sana shangazi yake. Humsaidia kazi za nyumbani kama vile kuosha vyombo, kufua na kufagia. Vilevile, humwagilia bustani ya maua. Nyumba yao inapendeza sana.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Fikiri anapokuwa shuleni, husoma kwa bidii. Anajua kusoma, kuandika na kuhesabu. Huwasaidia wanafunzi wenzake ambao huhitaji msaada. Rafiki yake Fikiri anaitwa Tumaini. Tumaini alikuwa hawezi kuhesabu vizuri lakini Fikiri alimsaidia. Siku hizi Tumaini anaweza kuhesabu vizuri. Walimu na wanafunzi wanampenda sana Fikiri.

Fikiri ni mwanafunzi m**tii**fu. Hutekeleza maelekezo anayopewa na wazazi au walezi na hata wanafunzi wenzake. Anapokuwa shuleni huwa**heshimu** walimu na viongozi wote. Fikiri ni mfano bora wa ku**igwa**.

Siku moja, Fikiri alikuwa anatoka shuleni kuelekea nyumbani. Njiani alikutana na bibi mmoja. Bibi alikuwa amebeba kuni kichwani na **kikapu** mkononi. Fikiri alimsalimia kisha akamwambia, "Bibi naomba nikusaidie kubeba kikapu."

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 65 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Bibi alifurahi sana. Akajibu salamu na kumpa kikapu, kisha wakaendelea na safari. Walipofika **njiapanda** Fikiri akamwambia bibi, "Mimi ninaelekea barabara iendayo kulia." Bibi akamwambia Fikiri, "Asante sana mjukuu wangu. Mimi ninaelekea barabara iendayo kushoto." Bibi alichukua kikapu chake na kumshukuru Fikiri. Kisha kila mmoja aliendelea na safari yake.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Fikiri anasoma shule gani?
2. Nani alimsaidia Tumaini kujua kuhesabu?
3. Kwa nini Fikiri ni mfano wa kuigwa?
4. Kwa nini bibi alimshukuru Fikiri?
5. Habari hii inatufundisha nini?



KISWAHILI DARASA 3.indd 66 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana za maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano: kikapu** - *chombo cha kubebea vitu*

*Babu ameweka mihogo ndani ya kikapu.*

*Mama anasuka kikapu kizuri.*

1. kitindamimba
2. tii
3. heshimu
4. iga
5. kikapu
6. njiapanda

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Andika NDIYO kwenye sentensi ya kweli au HAPANA kwenye sentensi isiyo ya kweli.**

(i) Wanafunzi hawapaswi kuwasaidia wazazi wao kazi za nyumbani. ________

(ii) Wanafunzi wanaweza kufundishana. ________

(iii) Fikiri ni mtoto mwenye tabia nzuri. ________

(iv) Hatupaswi kuiga tabia ya Fikiri. ________

(v) Fikiri ni mwanafunzi mtiifu. ________

(vi) Bibi alimsifu Fikiri kwa tabia yake mbaya. ________

(vii) Fikiri ni mfano bora wa kuigwa. ________

(viii) Shangazi ni ndugu wa kike wa baba. ________

**B. Chagua jibu sahihi na kuliandika sehemu iliyoachwa wazi:**

(i) Fikiri ni kitindamimba katika familia yao. Maana yake ni ............

(a) mtoto wa kwanza kuzaliwa

(b) mtoto wa pili kuzaliwa ( )

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) mtoto wa mwisho kuzaliwa
(d) mtoto wa kati kuzaliwa

(ii) Wewe ni mwanafunzi unayetekeleza yale unayoambiwa. Kwa hiyo wewe ni nani?
(a) mtiifu
(b) mkorofi ( )
(c) mtukutu
(d) mwongo

(iii) Nini maana ya kutoa msaada?
(a) kumpa mtu zawadi
(b) kumpongeza mtu ( )
(c) kumsaidia mtu
(d) kumshukuru mtu

(iv) Jamila amezaliwa tumbo moja na baba yako. Unamwitaje Jamila?
(a) mjomba
(b) shangazi ( )
(c) binamu
(d) bibi

**C. Soma sentensi zifuatazo kwa umakini, kisha pigia mstari neno lililokosewa.**
(i) Fikiri ni wanafunzi wa Darasa la Tatu.
(ii) Watoto wanapaswa kumheshimu wazazi.
(iii) Mwanafunzi wote wamefungua shule.
(iv) Dada na kaka anaimba wimbo.
(v) Bibi walikuwa amebeba kuni na kikapu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi:**

(i) Watoto anacheza mpira.
(ii) Machungwa mazuri limeiva.
(iii) Kitabu yangu kimechanika.
(iv) Baba na mama anapika jikoni.
(v) Maembe yote limeoza.
(vi) Majina aliyoitwa ni erika asha na edithi.

## Kazi ya kufanya

**Katika kikundi chagueni hadithi mbili, kisha msomeane kwa kuzingatia muda mliopangiwa na kuulizana maswali kuhusu hadithi mlizosoma.**

## Zoezi la 4: Utungaji

**Panga sentensi zifuatazo kwa mtiririko sahihi.**

1. Kengele ya kukusanyika ililia na mwalimu wa zamu alitoa matangazo.
2. Siku hiyo wanafunzi waliwahi kufika shuleni.
3. Walipoingia tu, walianza kujifunza wakiongozwa na walimu.
4. Walifanya usafi wa mazingira vizuri kwa kuongozwa na viranja.
5. Baada ya matangazo wanafunzi walielekea darasani kwa ukakamavu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Ninaweza kuandika

**Utangulizi**

*Katika sura hii, utajifunza kuandika habari na hadithi fupi. Pia, utajifunza kufuata kanuni na taratibu za uandishi wa habari na hadithi. Maarifa utakayoyapata yatakuwezesha kuwa mwandishi mzuri katika maisha ya kila siku.*

**Fikiri**

Jinsi habari na hadithi zinavyoandikwa

**Ufahamu**

**Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**

### Siku ambayo sitaisahau

Ilikuwa siku ya Jumanne ya tarehe 5 Septemba mwaka 2023 ambayo sitaisahau maishani mwangu. Siku hiyo nilitokea maeneo ya Dumila, mkoani Morogoro kuelekea Manyovu, mkoani Kigoma. Tulisafiri kwa gari dogo binafsi lililokuwa likiendeshwa na mjomba wangu Bwana Jedio.

Tulipita Dodoma mpaka Tabora. Kwa kipindi chote cha safari, gari letu lilikuwa shwari kabisa. Tulikuwa tunaenda kwenye **mahafali** ya vijana waliokuwa wanahitimu mafunzo mafupi ya Jeshi la Kujenga Taifa. Usilolijua ni kama usiku wa giza. Kumbe ilikuwa siku ya **balaa**, tena ya bahati mbaya kwetu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tulipokaribia Wilaya ya Urambo, dereva wetu alianza kuendesha kwa mwendo wa **kasi** bila ya kuchukua tahadhari ya kutosha. Ndani ya gari hilo tulikuwemo **abiria** tusiopungua watano. Wote tulikuwa tumefunga mikanda, tunaenda kwenye mahafali hayo kushuhudia gwaride, maonesho na mambo mengine mengi ya kijeshi.



Lahaula! Tulipofika njiapanda ya Urambo, tulikutana na lori kubwa la mchanga maarufu kama mende. Lori hilo liliingia kwenye barabara kuu kwa kasi bila ya dereva kuruhusiwa na taa za upande wake. Puuu! Kilikuwa ni kishindo kikubwa kama bomu. Watu walipiga mayowe wakisema, “Ajaliii!!” Wengine walisema, “Mungu wangu!” Wengine waliita, “Mamaaa!!” Kelele nyingi zilisikika.



KISWAHILI DARASA 3.indd 71 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ilikuwa **ajali** mbaya ambapo gari letu liligongwa na lori na kuburuzwa hadi mtaroni. Vioo vyote vilipasuka na gari lilibonyea maeneo mengi. Abiria wote tulipata majeraha madogo.

Polisi waliwahi eneo la tukio na kushirikiana na raia wema kuokoa watu. Magari mawili ya polisi yalitumika kuwawahisha majeruhi kwenye hospitali kubwa iliyokuwa jirani na eneo la tukio. Madaktari na wauguzi walipambana kuokoa **maisha** ya majeruhi hao. Baada ya muda mfupi tulikuwa tumepatiwa matibabu na kuruhusiwa. Hakika hii ni siku ambayo sitaisahau kamwe!

Jambo nililojifunza ni kuwa kila raia anapaswa kufuata sheria za usalama barabarani. Sheria hizi zinatulinda wote.

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Abiria waliopata ajali walikuwa wakielekea kwenye tukio gani?
2. Dereva wa gari lipi alikuwa mzembe? Eleza uzembe wake.
3. Kuna umuhimu gani wa kuwaokoa kwa haraka wasafiri waliopata ajali?
4. Nini maana ya raia wema?
5. Madereva hupaswa kuchukua tahadhari gani wanapoendesha magari?
6. Habari hii inatufundisha nini?
7. Andika habari hii kwa maneno yako mwenyewe kwa sentensi tano (5)

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana za maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano: abiria** – *mtu/watu wanaosafiri kwa chombo cha usafiri*

*Abiria wote waliambiwa wafunge mikanda.*

*Abiria waliopanda treni ya mwendokasi walifika haraka.*

1. mahafali
2. balaa
3. kasi
4. abiria
5. ajali
6. maisha

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Tunga sentensi kumi kwa kutumia jedwali lifuatalo:**

**Mfano:** *(i) Kaka hapendi ugomvi.*

*(ii) Darasa letu hupambwa kwa picha mbalimbali.*

| | | |
|---|---|---|
| Kaka | hupambwa kwa | madawa ya kulevya |
| Madawa ya kulevya | hufunzwa na | vizuri |
| Mwalimu wetu | hushusha | ugomvi |
| Mtoto mwema | ni hatari | wazazi |
| Darasa letu | hapendi | maadili ya nchi yetu |
| | ni haramu kwa | walimu |
| | hutufundisha | picha mbalimbali |
| | ni aina ya | kelele |
| | | kwa afya zetu |
| | | maua |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B. Panga herufi zifuatazo ili kupata maneno sahihi.**

**Mfano:** SHOEK - *KESHO*

| | |
|---|---|
| (i) MAIUT | (iv) VYELA |
| (ii) KOTOKO | (v) MUNBANYI |
| (iii) ZAATKA | (vi) RUMAHA |

**C. Panga maneno yafuatayo ili kupata sentensi sahihi.**

(i) mwerevu mwalimu darasani mwanafunzi humwelewa
(ii) bidii kwa mtihani tutafaulu tukisoma
(iii) mnyama porini ni anayeishi mbweha
(iv) nilipewa nilipofaulu mtihani zawadi
(v) maua darasa hupambwa mazuri letu kwa sana
(vi) saba ina siku moja wiki

**D. Panga sentensi zifuatazo katika mtiririko unaofaa.**

(i) Anaishi na wazazi wake katika Kijiji cha Lihole.
(ii) Waliwahi zahanati ya karibu kupatiwa matibabu.
(iii) Mama yake alichimba viazi na yeye alikuwa akivitia kapuni.
(iv) Siku moja yeye na mama yake walikwenda shambani kuchimba viazi.
(v) Kwa bahati mbaya nyuki waliwavamia na kuwajeruhi.
(vi) Lipake ni mwanafunzi anayesoma Darasa la Tatu.

**Kazi ya kufanya**

**Soma habari au hadithi, kisha andika kwa ufupi habari au hadithi hiyo.**

**Zoezi la 4: Utungaji**

**Tunga habari fupi yenye kichwa cha habari "Chakula ninachokipenda" kwa kuzingatia mpangilio sahihi wa maneno na alama za uandishi.**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

## Kuchambua matini

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza kuchambua matini ili kueleza mambo mazuri na mabaya. Pia, utajifunza mambo ya kuzingatia katika uchambuzi wa matini. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuchambua matini mbalimbali kama vile hadithi, habari, mazungumzo na mashairi katika maisha yako ya kila siku.*



**Fikiri**

Mambo mbalimbali ambayo unaweza kupata ukisoma habari.

**Ufahamu**

**Soma shairi na habari, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Shairi**

**Tuyatunze mazingira**

1. Leo tumekusanyika, **mazingira** kuyajua,
   Mama baba nawe kaka, ni vema mkasogea,
   Ili nipate sikika, kisha nanyi tachangia,
   Sipotunza mazingira, nayo hayatatutunza.

2. Tukitunza mazingira, **faida** tajipatia,
   Tutaepuka madhara, kamwe maradhi sikia,
   Tutapata afya bora, hewa safi nakwambia,
   Sipotunza mazingira, nayo hayatatutunza.

3. Miti hutusaidia, kwa mbao matunda pia,
   Kivuli hutupatia, mvua kutuletea,
   **Mmomonyoko** zuia, ardhi itatulia,
   Sipotunza mazingira, nayo hayatatutunza.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Mazingira kuyatunza, faida tumezijua,
Taka wengi kutotunza, sasa acha nakwambia,
Mana hili si la kwanza, sote tuiweke nia,
Sipotunza mazingira, nayo hayatatutunza.

## Habari



Watu wote katika familia hupaswa kutunza **mazingira**. Tukitunza mazingira yetu tutapata **faida** nyingi. Tutapata hewa safi, tutaepuka **maradhi** na tutakuwa na afya bora. Miti hutupatia mbao, matunda, kivuli na mvua. Vilevile, miti huzuia **mmomonyoko** wa udongo. Tuache tabia ya kutupa takataka ovyo kwa kuwa zinachafua mazingira.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Nani anayepaswa kutunza mazingira?
2. Taja faida tunazozipata kwa kutunza mazingira.
3. Eleza nini kitatokea tukiishi katika mazingira machafu.
4. Wewe unafanya shughuli gani za kutunza mazingira?
5. Taja idadi ya beti katika shairi la "Tuyatunze mazingira."
6. Eleza ujumbe unaoupata katika ubeti wa pili na wa nne.
7. Eleza hasara tunazozipata kwa kutokutunza mazingira.
8. Eleza tofauti katika usomaji wa shairi na habari.
9. Pendekeza kichwa cha habari hii.

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana za maneno yafuatayo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano: mazingira** - *ni jumla ya vitu vinavyomzunguka mtu katika makazi yake*

*Mazingira machafu huleta magonjwa.*

*Shule yetu ina mazingira mazuri.*

1. mazingira
2. faida
3. maradhi
4. mmomonyoko

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua neno sahihi katika maneno haya.**

| |
|---|
| mazingira, madhara, kufyeka, mmomonyoko, jitihada |

(i) __________ ni hali ya kuondolewa kwa udongo kunakosababishwa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na maji au upepo.

(ii) __________ ni kukata miti au nyasi ili ziwe fupi.

(iii) __________ ni matokeo yanayosababishwa na uharibifu wa kitu fulani.

(iv) __________ ni bidii ya kufanya jambo.

(v) __________ ni jumla ya vitu vinavyomzunguka binadamu.

**B. Tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

(i) ardhi
(ii) kivuli
(iii) hewa
(iv) matunda
(v) afya

**C. Andika kinyume cha maneno haya.**

(i) chafu
(ii) hasara
(iii) dondosha
(iv) tunza
(v) kusanya

**Kazi ya kufanya**

**Soma vitabu vya hadithi vitatu kutoka katika vyanzo mbalimbali, kisha andika mafunzo ya hadithi hizo.**

**Zoezi la 4: Utungaji**

**Tunga habari, kisha eleza mafunzo ya habari hiyo.**

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 78 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

## Kusimulia hadithi

### Utangulizi

*Katika sura hii, utajifunza namna ya kusimulia hadithi. Pia, utajifunza namna mbalimbali ya kuanza na kumalizia hadithi hizo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kusimulia hadithi kwa ufundi na kwa kujiamini. Vilevile, utaweza kuelimisha, kufurahisha na kuburudisha wasikilizaji.*

### Fikiri

Mambo yanayokuvutia katika hadithi.

**Ufahamu**

**Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Ndege wetu**

Hapo **kale**, palitokea ndege wengi waliokuwa wamejawa na furaha. Kila mmoja alim**tambia** mwenzake kuhusu sifa alizonazo katika jamii. Wengine walitamba kuhusu rangi zao, umbile lao na sifa nyingine nyingi. Kuku alianza kutamba na Bundi akamalizia kama ifuatavyo:

Kuku Jike alianza kwa kutamba kuwa yeye ni jamii ya ndege. Hu**taga** mayai na ku**angua** vifaranga. Mayai ni chakula bora. Kuku Dume ambaye ni Jogoo alieleza kuwa yeye huwika mapema asubuhi. Watu wengi huamshwa na sauti yake. Kuku walimaliza

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

bila kuitaja sifa yao moja kubwa kuwa nyama yao hupendwa na watu wengi.



Mwewe naye aliingia kwa mbwembwe na alieleza kuwa yeye huishi juu ya miti. Mara nyingi hupenda kuruka kutoka mti mmoja kwenda mwingine. Mwewe alisema chakula chake ni vifaranga vya kuku.





KISWAHILI DARASA 3.indd 80 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kasuku hakuwa nyuma. Naye aliingia na kueleza kuwa yeye ni ndege mwenye rangi nyingi. Anapenda kuiga sauti za binadamu. Mara nyingi hufugwa na binadamu.



Majigambo yaliendelea Batamzinga na Mbuni walifuata. Batamzinga alisema yeye ni ndege wa porini, pia hufugwa. Alijilinganisha ukubwa wake na kuku. Batamzinga alitamba kuwa yeye ni mkubwa kuliko kuku. Pia, ana rangi nyingi na hupenda kula samaki.



FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 81 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mbuni yeye aliingia kwa **madaha**. Alijieleza kuwa yeye ni ndege mkubwa mbugani. Hivyo, hawezi kuruka juu sana ila ana uwezo wa kukimbia sana. Mbuni hutaga mayai makubwa sana.



Siku ile ndege wote walikuwa na furaha. Kila ndege alikuwa akionesha **mikogo** kwa kuyapigapiga mabawa yake. Kunguru, Chiriku na Bundi walikuwa wa mwisho kujieleza. Kunguru aliringa kwa rangi yake nyeusi. Kunguru alieleza kuwa baadhi yao wana doa moja jeupe shingoni. Wao hula vyakula mbalimbali.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Chiriku naye alitamba kwa kujiita kinanda wa angani. Yeye hula nafaka. Pia, ni ndege mwenye umbile dogo.



Bundi alimalizia kwa kusema kuwa yeye ana macho makubwa yanayomsaidia kuona vizuri usiku. Mara nyingi huonekana usiku.



FOR ONLINE USE ONLY

Ndege waliifurahia siku hiyo. Kila mmoja alijua sifa za mwenzake. Ingawa sifa nyingine zilikuwa za kuongeza chumvi. Baada ya hapo wote walitawanyika na kuendelea na majukumu mengine.



KISWAHILI DARASA 3.indd 83 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Ndege gani alianza kutamba?
2. Taja jina la ndege mkubwa kuliko wote.
3. Ndege gani alimalizia kutamba?
4. Umependa maelezo ya ndege gani? Kwa nini?
5. Habari hii inatufundisha nini?

## Zoezi la pili: Msamiati

**Eleza maana za maneno yafuatayo na tunga sentensi mbili kwa kila neno.**

**Mfano: kale** - *zamani sana*

*Hapo kale binadamu waliishi mapangoni.*

*Hapo kale wanyama wote waliishi porini.*

1. kale
2. tamba
3. taga
4. angua
5. madaha
6. mikogo

## Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

**A. Andika NDIYO kwenye sentensi ya kweli au HAPANA kwenye sentensi isiyo ya kweli.**

(i) Batamzinga ni mkubwa kuliko kuku.____________

(ii) Chiriku ana macho makubwa kuliko bundi. ____________

(iii) Kunguru ni mdogo kuliko mbuni. ____________

(iv) Kasuku ana mdomo mrefu kuliko kunguru. ____________

(v) Bundi mara nyingi huonekana mchana. ____________

(vi) Mayai ya kuku ni makubwa kuliko ya mbuni. ____________

**B. Panga herufi zifuatazo ili kupata neno sahihi.**

(i) IUBND ____________

(ii) RUKICHI ____________

(iii) NUKUGUR ____________

(iv) KUSAKU ____________

(v) THAHIDI ____________



FOR ONLINE USE ONLY

KISWAHILI DARASA 3.indd 84 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufahamu

**Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

### Urafiki wa uongo



Hapo zamani, kulikuwa na Kuku na Mwewe. Kuku na Mwewe walikuwa marafiki sana. Kuku alikuwa na watoto watano na Mwewe alikuwa na watoto watatu. Wote walikuwa wanapenda kucheza pamoja. Siku moja kulitokea njaa, Mwewe akamwambia Kuku waende porini kuwinda. Kuku alikubali na waliwaacha watoto na kuelekea porini. Watoto wa mwewe walikaa juu ya mti na wa kuku chini ya mti.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kuku na Mwewe walianza safari. Walipokuwa njiani, Mwewe alimwambia Kuku kuwa amesahau manati yake. Hivyo, anarudi kuyachukua. Kumbe Mwewe alimdanganya Kuku.

Mwewe alianza safari ya kurudi nyumbani. Kuku alimsubiri Mwewe akidhani kuwa atarudi mapema. Kuku alikaa kwa muda mrefu lakini Mwewe hakurudi. Baadaye, Kuku aliamua kuanza safari ya kurudi nyumbani. Alipofika, alimkuta Mwewe amekaa juu ya mti na watoto wake. Kuku alimuuliza, "Rafiki yangu Mwewe watoto wangu wako wapi?" Mwewe akamjibu, "Nimewageuza chakula changu." Kuku alikasirika sana na kumchukia Mwewe. Hadi leo kuku na mwewe ni maadui.

## Zoezi la 4: Ufahamu

1. Nani walikuwa marafiki?
2. Kuku na Mwewe walikubaliana kwenda wapi?
3. Mwewe alimdanganya nini Kuku? Kwa nini alifanya hivyo?
4. Kitu gani kiliwatokea watoto wa Kuku?
5. Kwa nini Kuku alikasirika sana na kumchukia Mwewe?
6. Hadithi hii inatufundisha nini?
7. Simulia hadithi hii kwa maneno yako mwenyewe.

## Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

**A. Andika umoja au wingi wa maneno yaliyomo katika jedwali.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| (i) ndege | ____________ |
| (ii) ____________ | viota |
| (iii) ____________ | majani |
| (iv) mti | ____________ |
| (v) ____________ | mimea |
| (vi) mbuni | ____________ |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| (vii) ____________ | marafiki |
| (viii) mtoto | ____________ |

**B. Andika MWANZO kwa maneno yanayoanza katika hadithi na MWISHO kwa maneno yanayoishia katika hadithi.**

**Mfano:** Hapo zamani kulikuwa na marafiki wawili waliopendana. MWANZO

Tangu siku hiyo wanaishi kwa amani. MWISHO

(i) Paukwa! ________

(ii) Hadithi yangu imeishia hapo. ________

(iii) Hadithi hadithi! ________

(iv) Waliishi kwa raha mstarehe. ________

(v) Tangu siku hiyo walianza kuheshimiana. ________

(vi) Mshika mbili moja humponyoka. ________

(vii) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. ________

(viii) Hapo zama za kale palitokea sungura na fisi. ________

**C. Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza faida za kuitikiwa wakati unasimuliwa hadithi.
2. Wakati gani unapopaswa kumwitikia msimuliaji?

**D. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyopo kwenye kisanduku.**

| | | |
|---|---|---|
| ndege | samaki | mimea |
| matunda | nguo | nafaka |

(i) Perege, sangara, sato na kambare ni ___________.

(ii) Kanga, kasuku, kunguru na njiwa ni ___________.

(iii) Chungwa, embe, papai na tikiti ni ___________.

(iv) Mahindi, uwele, mtama, ulezi ni ___________.

(v) Suruali, gauni, sketi na shati ni ___________.

(vi) Mwembe, mgomba na mchungwa ni ___________.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 87 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya Kufanya

**Soma na igiza ngonjera ifuatayo:**

**Tanzania katika ukombozi wa Afrika**

**Tunu**
Hodi hodi uwanjani, kwa furaha naingia,
Furaha iso kifani, wakoloni kuwatoa,
Nyerere msitarini, uhuru kupigania,
Uhuru wa Afrika, Tanzania furahia.



**Musa**
Dada we' kwanza tulia, niyaweke mambo wazi,
Wakoloni hurumia, si nguvu za viongozi,
Hawakutaka umia, kuutoa ukombozi,
Hiari waliamua, kutupatia uhuru.

**Tunu**
Kaka acha usingizi, kweli mengi huyaoni,
Afrika viongozi, watoka usingizini,
Neto kang'oa mizizi, ya wakoloni shimoni,
Uhuru wa Afrika, Angola wafurahia.



**Musa**
Yahitajika elimu, dada kukuelimisha,
Viongozi kuhujumu, singeweza kutupasha,
Huruma yao adhimu, uhuru kuupitisha,
Hiyari waliamua, kutupatia uhuru.

**Tunu**
Samora sitosahau, Wareno walimkoma,
Uhuru kuweka dau, porini alisimama,
Na hakuleta dharau, sauti kuunguruma,
Uhuru wa Afrika, Msumbiji furahia.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kuna Robert Mugabe, Zimbabwe akainua,
Akatangaza ubabe, walowezi kuwang'oa,
Usia wao tubebe, mkoloni kumtoa,
Uhuru wa Afrika, Zimbabwe wafurahia.



**Musa** Sioni walokifanya, hao nilowabaini,
Hata nguvu ngekusanya, singeshinda wakoloni,
Mali nyingi likusanya, Afrika maskini,
Hiari waliamua, kutupatia uhuru.

**Tunu** Mandela kafanya kazi, imara bila ajizi,
Kweli alipiga mbizi, kutafuta mageuzi,
Alipinga ubaguzi, kwa hasira ya mkizi,
Afrika ya Kusini, uhuru wafurahia.



**Musa** Sasa nimekuelewa, juhudi za viongozi,
Elimu kubwa tolewa, na Nujoma kiongozi,
Namibia piganiwa, Afrika mapinduzi,
Tanzania hakubaki, nao pia lishiriki.



**Tunu** Kuna kambi ya Mazimbu, Morogoro ilikaa,
Nayo Kongwa kumbukumbu, ukombozi ilizaa,
Bado kuna kumbukumbu, kule Chunya walikaa,
Tanzania kuongoza, ukombozi Afrika.

Nachingwea walikaa, Msumbiji walotoka,
Mreno walikataa, kwa mapanga na mashoka,
Vita ikatapakaa, mkoloni kapigika,
Nchi zote za kusini, msaada tulitoa.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI DARASA 3.indd 89 02/12/2023 18:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tanzania iliwapa, vifaru nazo bunduki,
Chakula chote cha hapa, mishale hata mikuki,
Askari tuliwapa, vitani wakashiriki,
Tanzania ni kinara, hapa kwetu Afrika.

**Wote** Pamoja tunakubali, mchango wa Tanzania,
Nchi nyingi mbalimbali, Tanzania saidia,
Namibia nayo kweli, uhuru lipigania,
Afrika ya Kusini, uhuru yafurahia.

## Zoezi la 6: Utungaji

**A. Malizia hadithi ifuatayo:**

Paukwa! ...

Hapo zamani za kale katika kijiji cha Nkona kulikuwa na vijana watatu watundu sana. Vijana hawa waliitwa Ndevu, Kinono na Chapale. Chapale alikuwa mrefu kama twiga huku Ndevu na Kinono wakiwa warefu wa kawaida. Siku moja vijana hawa walikwenda kuvua samaki kwenye mto Luiche.

Walipokuwa wakivua, ...

**B. Ongeza ubeti katika shairi lifuatalo:**

Siku yetu imefika, la tatu tunaliaga,
Walimu wametupika, umahiri umenoga,
Tulijifunza hakika, vitendawili kutega,
Furaha iso kifani, tunaingia la nne.

FOR ONLINE USE ONLY

## Vitabu kutoka
## Taasisi ya Elimu Tanzania

### Darasa la Tatu




























ISBN 978-9987-09-877-4